HOTUBA YA MH. DKT. ANNA E. MGHWIRA, MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO KWENYE UZINDUZI WA KAMPENI YA "FURAHA YANGU" YA KUHAMASISHA WANANCHI HUSUSANI WANAUME KUPIMA VVU NA KUANZA KUTUMIA DAWA MAPEMA KWA WENYE MAAMBUKIZI YENYE KAULI MBIU ISEMAYO "PIMA, JITAMBUE, ISHI"

KATIKA VIWANJA VYA SHREE HINDU MANDAL MOSHI

TAREHE 13 SEPTEMBA, 2018

- Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro
- Mh. Mkuu wa Wilaya ya Moshi
- Mh. Mwenyekiti wa CCM Mkoa
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya;
- Waheshimiwa Wabunge mliopo hapa;
- Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri;
- Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI;
- Wakurugenzi wa Halmashauri;
- Viongozi wa Madhehebu ya Dini
- Viongozi Wakuu na Watendaji wa Serikali
- Viongozi wa Vyama vya Siasa;
- Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI,
- Wadau wa Maendeleo katika Mapambano dhidi ya UKIMWI.
- Waandaaji wa Kampeni ya "*FURAHA YANGU" PIMA, JITAMBUE, ISHI*";
- Waandishi wa Habari;
- Wageni Waalikwa; Mabibi na Mabwana:

Ndugu Wananchi;

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema na kutukutanisha pamoja katika uwanja huu ili kushiriki katika tukio hili muhimu la uzinduzi wa kampeni ya **"Furaya Yangu"** yenye kauli mbiu isemayo **"Pima, Jitambue, Ishi".** Kampeni hii inalenga kuhamasisha wananchi hususani wanaume kupima VVU na kwa waliogundulika kuwa na VVU kuanza kutumia dawa za kufubaza VVU (ARV) mapema. Kitaifa kampeni hii ilizinduliwa na Mh.Waziri Mkuu (Mb) wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 19 Juni, 2018 huko Makao makuu ya nchi Jijini Dodoma.

Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP), Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) na TAMISEMI kwa kuratibu kampeni hii Kitaifa na kutoa miongozo ya jinsi ya kufanya uzinduzi kwa ufanisi katika ngazi za Mikoa. Uzoefu wa uzinduzi wa kampeni hii uliofanywa Kitaifa umetoa hamasa kwa jamii kuona umuhimu wa kushiriki na umesaidia kupata mafanikio tunayoyaona leo hii.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa kamati ya Mkoa ya maandalizi ya shughuli hii kwa kushirikiana na Wadau wa ndani ya Mkoa kwa jitihada zao zilizofanikisha uzinduzi wa kampeni hii. Pia natoa shukrani kwa Uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa kuwa mwenyeji wa uzinduzi huu na kwa ushirikiano mkubwa mliouonyesha katika kufanikisha uzinduzi wa Kampeni hii katika Mkoa wetu, **Hongereni sana!**

Ndugu Wananchi;

Kampeni hii inawalenga watanzania wote kutambua hali zao za maambukizi ya VVU, hususani **wanaume** na makundi mengine ambayo ni wasichana walio katika umri wa balehe, wanawake vijana wenye umri wa miaka 15-24, akinamama wajawazito na wanaonyonyesha pamoja na watoto wao.

Kampeni hii inawalenga wanaume zaidi na makundi tajwa hapo juu kwa sababu takwimu za utafiti wa **Viashiria na Matokeo ya UKIMWI Tanzania wa** mwaka 2016-2017 umeonyesha ni asilimia 52 tu ya watu wanaoishi na VVU wamepima na kujua hali zao za maambukizi ya VVU. Aidha takwimu hizi zinaonyesha kuwepo kwa kiwango cha chini cha upimaji wa VVU kwa wanaume (45.3 %) ukilinganisha na wanawake (55. 9%). Pia wanaume walio wengi wana mtizamo hasi wa kutafsiri majibu ya kipimo cha VVU cha wenza wao kwamba ndio majibu yao. Kiafya hali hii ni hatari sio tu kwa mtu binafsi bali pia kwa familia, kaya na Taifa kwa ujumla. Pia inadhoofisha juhudi za Serikali na Wadau wa mwitikio wa VVU na UKIMWI nchini kufikia malengo ya kitaifa ya 90-90-90 ifikapo 2020 na hatimaye sifuri tatu mwaka 2030.

Ndugu Wananchi,

Tanzania imekuwa miongoni mwa nchi zinazoonyesha mafanikio katika kupunguza maambukizi ya VVU kwa kiwango kikubwa. Takwimu za utafiti wa Viashiria na matokeo ya UKIMWI nchini wa mwaka 2016/2017 zimeonyesha kushuka kwa kiwango cha maambukizi kutoka asilimia 7 mwaka 2003/2004 mpaka kufikia asilimia 4.7. Haya ni matokeo ambayo yanaonyesha mafanikio mazuri dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI nchini.

Ndugu Wananchi,

Kufuatia mipango mbalimbali ya kimkakati na juhudi za wadau mbalimbali, kiwango cha maambukizi katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro kimeendelea kupungua kutoka asilimia 7.3 mwaka 2003/2004 hadi asilimia 2.6 mwaka 2016/2017 kwa mujibu wa takwimu za Utafiti wa Viashiria na Matokeo ya UKIMWI Tanzania wa mwaka 2016/2017. Matokeo haya yameuweka mkoa wa Kilimanjaro kuwa miongoni mwa mikoa yenye kiwango cha chini cha maambukizi nchini dhidi ya kile cha kitaifa cha asilimia 4.7. Aidha, kwa mujibu wa utafiti huu kiwango cha kufubaa kwa VVU kwa Mkoa wetu ni asilimia 67 dhidi ya asilimia 52 ya kitaifa. Matokeo haya yameuweka Mkoa wa Kilimanjaro kuwa wa pili kitaifa kwa kuwa na kiwango cha juu cha kufubaa kwa VVU ukitanguliwa na Lindi.

Ndugu wananchi

Napenda niwapongeza sana wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa kujitokeza kwa wingi kushiriki kwenye shughuli hii tangu ilipoanza tarehe 10 Septemba, 2018 na naamini mtandelea kuhamasishana kuja kupata ushauri na huduma zinazotolewa na wataalamu. Hii imedhirishwa na idadi ya watu waliojitokeza kupima afya zao ambapo tangu kampeni ilipoanza Mkoani kwetu hadi leo tumeweza kufikia watu .....kama ilivyoelezwa kwenye taarifa iliyotangulia. Natoa rai kuwa ni vizuri tuwe na desturi ya kupima afya zetu ili tuweze kupata huduma stahiki kwa wakati.

Ndugu wananchi

Ninatumaini kwamba wengi wetu, mnajua Kampeni ya "**FURAHA YANGU"** ina kauli mbiu isemayo **" PIMA, JITAMBUE, ISHI"** hii ni kutokana na ukweli kwamba kampeni hii inatoa ujumbe wa furaha kwa wote watakaopima na kujua hali zao za maambukizi. Na kwa wale

watakaokutwa na maambukizi ya VVU, mchakato wa kuwaanzishia matibabu unaanza mara moja tofauti na ilivyokuwa zamani walipokuwa wanalazimika kusubiri hadi kinga zao (CD4) zishuke au kufikia hatua ya juu ya ugonjwa. WAVIU wakianza dawa za **ARV mapema na kuzitumia kama inavyotakiwa**, huweza kuishi maisha ya kawaida na kupunguza uwezekano wa kuwaambukiza watu wengine kutokana na ukweli kwamba dawa za ARV huimarisha kinga za mwili na kufubaza VVU. Hivyo basi, kauli mbiu ya kampeni hii inaleta furaha na amani kwa watu hata kama wanaishi na VVU.

Ndugu wananchi

Changamoto kubwa tuliyonayo kuhusu huduma ya Tiba na Matunzo ni kwa baadhi ya WAVIU kutokuwa na ufuasi mzuri wa dawa pindi hali zao kiafya zinapoonekana kuimarika. Nitoe rai kwa WAVIU wote waliokwisha anza kutumia dawa za ARV, wazingatie ufuasi wa dawa. Aidha wadau wote mhakikishe mnawashirikisha vyema WAVIU hasa waliojiweka wazi hali zao, katika kutoa ushuhuda na kuhamasisha WAVIU wasiokuwa na ufuasi mzuri katika matumizi ya dawa za kufubaza (ARV).

Ndugu Wananchi,

Baada ya uzinduzi huu wa leo, nitoe rai kwa Halmashauri zote za Mkoa wetu, kwa kushirikiana na wadau waliopo katika maeneo yenu, kufanya uzinduzi wa kampeni hii na kuendelea nayo kwa mfululizo hadi Novemba 30, 2018 ili kufikia lengo tulilojiwekea kupima watu wapatao 73,605. Wakuu wa Wilaya kwa kusaidiana na Wakurugenzi wa Halmashauri zetu zote msimamie kampeni hii kwa uzito unaostahili. Matokeo ya utekelezaji wa kampeni hii ya Mkoa wetu yanapaswa kuwasilishwa ngazi ya Taifa ili yatangazwe katika maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani Desemba Mosi 2018. Aidha matokeo ya utekelezaji wa Kampeni hii kutoka kwenye maeneo yenu yawasilishwe mkoani kila siku ili kuwezesha kufanya

tathmini ya utekelezaji. Kwa msingi huo, naagiza Waratibu wa UKIMWI ngazi ya Mkoa kwa kushirikiana na Wadau wa Masuala ya VVU na UKIMWI, mfanye ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha taarifa ya utekelezaji wa kampeni hii ngazi ya Halmashauri zinafika Mkoani kwa wakati ili kuweza kujumuisha taarifa zote na kuandaa taarifa ya Mkoa.

Ndugu Wananchi

Kwa vile suala la Takwimu ni muhimu sana ili kujua tumefanikiwa au la, naagiza kuwa kila Halmashauri ihakikishe inatoa taarifa ya matokeo ya utekelezaji wa Kampeni hii kwenye maeneo yenu wakati wa maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani Desemba Mosi Mwaka huu, kama ilivyokusudiwa. Aidha, natoa rai kwa Mganga Mkuu wa Mkoa kwa kushirikiana na Waganga Wakuu wa Wilaya, kuhakikisha vitendanishi na dawa za ARV zipo za kutosha katika kila kituo kinachotoa huduma katika Mkoa wetu.

Ndugu Wananchi

Napenda kuwahakikishia kuwa serikali yetu itaendelea kushirikiana na wadau pamoja na wafadhili wote wa ndani na nje ya nchi katika Mwitikio wa VVU na UKIMWI. Vilevile, nawahakikishia kwamba Serikali itahakikisha dawa zitaendelea kuwepo bila kukosa kwa hiyo natoa wito watu mjitokeze kupima afya zenu ili mfaidike na dawa za ARVs. Aidha napenda kuwafahamisha kuwa, wataalamu wetu wamejipanga vizuri, sio tu kupima VVU bali hata kutoa huduma nyingine zikiwemo uchangiaji wa damu salama, Afya ya Uzazi, uwiano wa uzito na urefu (Body Mass Index), magonjwa sugu yasiyoambukiza kama vile Kisukari na Shinikizo la Damu.

Ndugu Wananchi

Nimalizie hotuba yangu kwa kuwashukukuru wadau wote wa maendeleo wanaoleta misaada yao ya kifedha na kitaalamu katika Mwitikio wa VVU na UKIMWI Kilimanjaro na nchini kwa ujumla.

Aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru kipekee wadau wote wakiwemo EGPAF, Jhpiego, THPS, PACT,Tulonge Afya, MWAMI Foundation, TAWREF, Bonite Bottlers, Shree Hindu Mandal, Fountain Radio na Boma Hai Radio ambao wamechangia kufanikisha kampeni hii mkoani kwetu.

Ndugu Wananchi,

Baada ya kusema hayo, sasa natangaza kuwa kampeni ya kuhamasisha wananchi hususani wanaume kupima VVU imezinduliwa rasmi katika Mkoa wetu.

“FURAHA YANGU - PIMA, JITAMBUE, ISHI”

“MWANAUME JALI AFYA YAKO, PIMA VVU”

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA